TANGAZO LA SERIKALI NA 580 la tarehe 23/9/2022

SHERIA YA UTUMISHI WA UMMA,
(SURA YA 298)

# KANUNI

(*Zimetungwa chini ya kifungu cha 29(8)*)

KANUNI ZA MAREKEBISHO ZA KANUNI ZA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA SEKRETARIATI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA ZA MWAKA 2022

Jina

TS. NA. 326 of 2021

**1**. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Marekebisho za Kanuni za Uendeshaji wa Shughuli za Sekretariati ya Ajira katika Utumishi wa Umma za mwaka 2022 na zitasoma kwa pamoja na Kanuni za Uendeshaji wa Shughuli za Sekretariati ya Ajira katika Utumishi wa Umma za mwaka 2021 ambazo katika Kanuni hizi zitajulikana kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 9

**2**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 9 kwa kufuta kanuni ndogo ya (3) na kuandika upya kama ifuatavyo:

"(3) Waombaji watawasilisha maombi yao kati ya siku zisizopungua saba na zisizozidi siku kumi na nne isipokuwa kwamba, waombaji wa nafasi za watendaji wakuu na nafasi za uongozi za taasisi za kimkakati zitakazoainishwa na Katibu, watawasilisha maombi yao ndani ya siku ishirini na moja tangu kutolewa kwa tangazo."

Marekebisho ya kanuni ya 22

**3.** Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 22(5) kwa kufuta maneno "miezi sita" na baadala yake kuandika maneno "miezi kumi na mbili."

Marekebisho ya kanuni ya 37

**4.** Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 37(2) kwa kufuta maneno "Katibu atakapoamua vinginevyo" yanayojitokeza katika aya (b) na baadala yake kuandika maneno "kupita muda usiopungua miezi tisa na usiozidi miezi kumi na mbili".

Dodoma
…………………., 2022

HASSAN OMARI KITENGE
*Katibu Sekretariati ya Ajira katika Utumishi wa Umma*